

MASWALI NA MAJIBU

Kimeandikwa na:
Najmuddin Murawwij Tabasi

Kimetarjumiwa na:
Amiri Mussa Kea



ترجمة

أسئلة وأجوبة

تأليف

نجم الدين مروّج الطبسي



© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 - 70 - 6

Kimeandikwa na:
Najmuddin Murawwij Tabasi

Kimetarjumiwa na
Amiri Mussa Kea

Kupangwa katika Kompyuta na:
Hajat Pili Rajab.

Toleo la kwanza: Januari, 2011
Nakala:1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.alitrah.org

Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

1. Mtu wa mwanzo kuzuiwa kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w].....2
2. Hukumu ya kutabaruku kaburi la Mtume [s.a.w.w].....3
3. Kumuomba msaada asiyekuwa Mwenyezi Mungu [a.j].....6
4. Dalili inayoruhusu kuzuru Makaburi.....9
5. Hukumu ya wanawake kuzuru makaburi.....12
6. Hukumu ya swala na dua pembezoni mwa makaburi ya Mawalii.14
7. Hukumu ya kujengea makaburi.....17
8. Hukumu ya kuweka alama juu ya makaburi.....19
9. Kuweka nadhiri kwa watu wema na waumini.....22
10. Hukumu ya sherehe na maombolezo.....23
11. Ndoa ya Muta'a.....25
12. Kwa nini Mashia huachia mikono wakati wa kuswali.....27
13. Swala ya tarawehe asili yake ni ipi.....29
14. Je! Amirul-Muiminiina Ali bin Abu Talib [a.s] na Maimamu watakatifu waliswali tarawehe.....31
15. Je! Ibara: “Asswalatu khairu minan-naum” na “Hayya ala khair-il-a'mal” ni sehemu ya adhana.....33
16. Raja'a ni nini.....34



NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiajemi kiiwacho, *Pasokh be Barkhi Shubahat-e Madhhabi (Majibu ya Baadhi ya Maswali Yenye Utata)*. Sisi tumekiita, *Maswali na Majibu*.

Kitabu hiki kiko katika mtindo wa maswali na majibu. Haya ni maswali ambayo Waislamu wengi, hususan wale ambao sio wa madhehebu ya Shia, imma wanauliza au huwahusisha Mashia na baadhi ya matendo ambayo wao huyaona kuwa ni uzushi (bidaa) na kuwashutumu nayo.

Mwandishi wa kitabu hiki amekusanya baadhi ya maswali na shutuma hizo wanazotupiwa Mashia na kuyapanga maswali na shutuma hizo katika kitabu hiki kwa mpango wa maswali na majibu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahilikwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Amiri Mussa Kea kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

UTANGULIZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu


Sifa zote njema anastahiki Mola wa viumbe, kisha rehema na amani zimfikie mbora wa viumbe Mtume Muhammad [s.a.w.w] pamoja na Ahlul-Bayt wake watoharifu [a.s], hasa hasa Imam wetu wa kumi na mbili, Imam al-Hujja Ibn Hasan Al-Askari [a.s].

Kitabu kidogo hiki kilichobeba anwani “Maswali na Majibu” - ni baadhi ya majibu ya maswali yaliyoulizwa katika hadhara na vikao kadhaa mbali mbali ambavyo mtunzi alishiriki kujibu maswali hayo, kisha kamati maalum ikakaa na kuandaa na hatimaye kuwa kitabu, kwa hivyo kimeandaliwa kwa muhtasari sana pamoja na kutaja vitabu rejea vinavyotegemewa zaidi na Ahlu Sunna ili watu wengi wapate faida.

Matumaini yetu ni kwamba baada ya mpendwa msomaji kusoma na kuelewa vizuri utawafikishia wengine, na iwapo utapatikana utata au kutofahamika baadhi ya mambo unaweza kuwasiliana na mtunzi. Matarajio yangu hapo baadaye ni kujibu maswali hayo na yanayofanana na hayo kwa urefu, mapana na ufafanuzi zaidi.

Najmuddin Murawwij Tabasi
22 Mfunguo Saba 1422 H.

Maswali na Majibu



Maswali na Majibu

Maswali na Majibu ndani ya vitabu vya Ahlu Sunna

Swali 1: Je! ni mtu gani wa mwanzo kuzuiwa kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w]?

Jibu: Ni Hakim Naysabuuri [aliyekufa mwaka 405 H], imepokewa kutoka kwa Daudi bin Abu Salehe amenukuu hivi:

Siku moja Marwan bin Hakam alimuona mtu amekaa juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] akaenda kwa jazba akamkamata na kumnyanyua juu, kisha akamuuliza: Je! Unajua nini umekifanya? Makusudio yake yalikuwa kwa nini umezuru jiwe na hilo ndilo lililokuleta hapa! Kando kidogo alikuwepo mfanya ziyara mwingine Abu Ayub Answare ambaye ni mmoja wa masahaba wa Mtume [s.a.w.w] alimsikia akisema: “Ndio, najua ninachokifanya hapa, mimi sikuja kuzuru jiwe bali nimekuja kuzuru Bwana Mtume [s.a.w.w], nilimsikia Mtume [s.a.w.w] akisema: “Msiililie dini ya Mwenyezi Mungu iwapo viongozi wake ni wale wahusika, na pindi ambapo itakapoongozwa na watu wengine basi hapo lieni.”

Na la kushangaza ni kwamba hadithi hiyo imepokewa na Hakim na Dhahabi katika sahihi zao, na hilo ni tukio lililothibiti katika historia wala hakuna utata juu ya hilo, kwa hakika ni dhahiri shahiri jambo hilo limeeleweka kwa watu wote wala halina ubishi wala kipingamizi kwa yeyote, bila shaka asili ya fikra hiyo ya uzuiaji au ukatazaji wa kuzuru makaburi imeletwa na Bani Umayya hasa hasa Marwan bin Hakam, al-Hakam ambaye alifukuzwa Madina na Bwana Mtume [s.a.w.w].¹

¹ *Mustadrak Hakim*, Juz. 4, uk. 560.

Maswali na Majibu

Swali 2: Je! Kugusa, kutabaruku na kubusu kaburi la Mtume [s.a.w.w] imeruhusiwa kisheria? Je! limeelezwa hilo katika vitabu rejea vya Ahlu Sunna na yupo aliyefanya hivyo?

Majibu – i: Ndio, Fatimah Zahra [a.s] alifanya hivyo katika kaburi la Mtume [s.a.w.w] na beti kadhaa za mashairi alisoma.²

ii: Abu Ayubu Answare aliweka uso wake juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] na kutabaruku.³

iii: Bilal Mhabeshi alitabaruku juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] na aliugusisha mwili wake juu yake na huku akilia.⁴

iv: Abdallah bin Umar aliweka mkono wake juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] kwa lengo la kutabaruku.⁵

v: Ibn Munkadar - yeye ni miongoni mwa vizazi vilivyokuja baada ya masahaba – yeye pia aliweka uso wake juu ya ardhi na alisema: Wakati nilipopatwa na tatizo au usahaulifu, ulimi wangu ulinitangulia na kusema niende katika kaburi la Mtume [s.a.w.w] na kuomba ponyo huko.⁶

Swali 3: Je! Wanachuoni wa madhehebu manne wanakubali kugusa na kutabaruku juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] pia makaburi ya watu wema?

Jibu: Ndio, imepokewa kutoka kwa Ahmad bin Hambali rais wa madhehebu ya Hambali, Ramlu Shafii, Muhibbu Diin Twabari na Abu

² *Irshadus Saari*, Juz. 3, uk. 352.

³ *Mustadrak Hakim*, Juz. 4, uk. 560.

⁴ *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 1, uk. 358 na *Usudul-Ghaaba*, Juz. 1 uk. 208.

⁵ *Sherh Shifaa*, Juz. 2, uk. 199.

⁶ *Siyar Aalaam Nubalaa* Juz. 3, uk. 213.

Maswali na Majibu

Swaif Yamani - ambaye ni mmoja wa wanachuoni wakubwa wa Makka - aidha Zargani Maliki, Izaami Shafii na wengineo ambao wamepokea na kunukuu tukio hilo kwa urefu kama ifuatavyo:

1. Abdallah Ibn Ahmad bin Hambali anasema: Siku moja nilimuuliza baba yangu: Je! Ipo hukumu gani kuhusu kugusa, kutabaruku na kubusu kaburi la Mtume [s.a.w.w] kwa lengo la kupata thawabu? Baba yangu akasema: Hakuna tatizo lolote lile.⁷
2. Ramlu Shafii anasema: Kutabaruku kaburi la Mtume [s.a.w.w], la mwanachuoni au la walii ni jambo lililoruhusiwa kisheria, kwa hivyo kubusu na kukumbatia kaburi hakuna tatizo.⁸
3. Muhibbu Diin Twabari Shafii anasema: Kubusu na kuweka mkono juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] ni jambo lililoruhusiwa, aidha ni siira na mwenendo wa waislamu na wacha mungu.⁹
4. Imethibiti katika historia kwamba watu wa Madina walikuwa wakichukua udongo juu ya kaburi la Mtume [s.a.w.w] na la Sayyidina Hamza na kuuweka majumbani mwao ili wawe wanatabaruku, aidha zimepokelewa hadithi ambazo zinazoeleza kwamba udongo wa Madina ni tiba ya kila maradhi, huepusha ukoma na maumivu ya kichwa.

Mmoja wa watafiti anasema: Udongo uliopo katika eneo la kaburi la Hamza ni chemchem ya udongo safi wa haramu mbili [Makka na Madina] ambao umetengwa maalum, hali kadhalika hutumiwa kwa ajili ya kutibu maumivu ya kichwa.¹⁰

⁷ *Jaamiu fi ilal wa Maarifat Rijaal*, Juz. 2, uk. 32 na *Wafaul Wafa*, Juz. 4 uk. 1414.

⁸ *Kanzul-Matwalib* uk. 219.

⁹ *Isnul-Matwalib*, Juz. 1, uk. 331.

¹⁰ *Wafaul-Wafa*, Juz. 1, uk. 69.

Maswali na Majibu

Abu Salama amepokea kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] amesema: “Vumbi la Madina huponya ukoma.”

Vile vile ananukuu Ibn Athiir Jazri hadithi kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] amesema: “Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, hakika udongo wake [Madina] ni ponyo la kila maradhi.”

Samahudi katika kitabu chake anaandika hivi: Siira na mwenendo wa Masahaba na watu wengineo ulikuwa kuchukua udongo uliopo kati-ka eneo la kaburi la Mtume [s.a.w.w] kwa ajili ya kutabaruku.¹¹

Swali 4: Toa mfano ambao unaonyesha kwamba Ahlu Sunna walikuwa wakitabaruku jeneza au kaburi la mmoja wa watukufu wao kwa lengo la kupata baraka?

Jibu: Zipo sehemu mbili ambazo hupigiwa mfano sana katika nadharia yenu nazo ni:

i. Kutabaruku udongo uliopo katika kaburi la Sahaba Saad bin Maadhi.

Ibn Saad na Dhahabi wanasema: Mtu mmoja alichukua udongo juu ya kaburi la Saad bin Maadhi, kisha akawaangalia na kujipakaza.¹²

ii. Kutabaruku udongo wa kaburi la Abdallah bin Hamdani.

Abu Naiim Isfahani na Ibn Hajar Askalaani wanasema: Hamdani ali-uawa mfungo tatu mwaka wa 183H, na watu wakamzika - siku ya tar-

¹¹ *Wafal-Wafa*, Juz. 1, uk. 544.

¹² *Twabaqaatul-Kubra*, Juz. 3, uk. 10 na *Siyar Aalam Nubalaa*, Juz. 1, uk. 289.

Maswali na Majibu

wiya - watu walifurika katika kaburi lake, basi wakaweka nguo na shati lake.¹³

Swali 5: Je! inafaa kumuomba msaada asiyekuwa Mwenyezi Mungu?

Jibu: Iwapo mtu anasema: Ewe Muhammad nikidhie haja au maombi yangu, hali ya kuwa makusudio yake kupata shufaa, au ana muomba Mwenyezi Mungu kupitia yeye hakuna tatizo, au anamuomba Mtume [s.a.w.w] ili yeye amuombee kwa Mwenyezi Mungu kwani zipo aya lukuki ndani ya Qur’ani tukufu ambazo zinatoa ishara juu ya hilo, baadhi ya aya hizo ni:

1. “...waruzuku hao na wavishe ...”¹⁴
2. “Na wala haikuwa nongwa kwao isipokuwa Mwenyezi Mungu amewaruzuku na Mtume wake...”¹⁵
3. “Na lau wao wangeliridhia aliyowapa Mwenyezi Mungu na Mtume wake...”¹⁶

Pamoja na kuwa kiumbe hahitaji kutoka kwa yeyote isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu pekee, lakini aya zilizotangulia hapo juu zinaonyesha kwamba Mwenyezi Mungu [s.w.t], Mtume [s.a.w.w] na waumini pia wao huruzuku na hushiriki katika kukidhi haja, wala hakuna tatizo lolote kwa hilo, ukiongezea kwamba masahaba pindi walipopatwa

¹³ *Hilyatul-Auliyaa*, Juz. 2, uk. 258, *Tahdhiib Tahdhiib*, Juz. 5, uk. 310, bila shaka rejea kaburi la Bukhari lililopo Samarkandi, na vile vile Ibn Taymiyya amenukuu maelezo hayo, rejea *Twabaqaatul-Shafiya*, Juz. 2, uk. 233, *Siyar Aalaam Nubalaa* Juz. 12, uk. 467 na *Bidaya wa Nihaya*, Juz. 14, uk. 136.

¹⁴ Sura 4 aya 5.

¹⁵ Sura 9 aya 74.

¹⁶ Sura 9 aya 59.

Maswali na Majibu

na matatizo mbali mbali walikuwa wakienda kwenye kaburi la Mtume [s.a.w.w] na kutawasuli kwake, bila shaka mtu mwenye akili timamu hukubali hilo, kwani katika zama za Khalifa wa pili Umar bin Khatwab watu walipatwa na janga la ukame, mmoja kati ya masahaba akaenda kwenye kaburi la Mtume [s.a.w.w] na akamuomba Mwenyezi Mungu kupitia Mtume [s.a.w.w] hapo alisema: “Ewe Mwenyezi Mungu uletee mvua umma wetu kwa baraka za Mtume Wako, kwani wanaangamia...”¹⁷ wengine waliofanya hivyo ni Ibn Nabban, Ibn Khuzaymah, Abu Ali Khilal na Sheikh wa madhehebu ya Hambali katika zama za janga la ukame ambapo walikwenda kwenye kaburi la Mtume [s.a.w.w] na kisha kumuomba Mwenyezi Mungu [s.a.w.w] kupitia Mtume Wake ili awaondolee balaa hilo.

1. Ibn Habban ambaye amekufa mwaka 350 H, katika kitabu chake “*Thiqaat*” anasema: Nilikwenda mara nyingi kwenye kaburi la Ali bin Musa Ridhaa [a.s] lililopo Tuus, kila nilipopatwa na shida nilikwenda kuzuru kaburi lake, na Mwenyezi Mungu [s.w.t] aliniondolea matatizo yangu, namshukuru Mola Manani kunitatulia matatizo niliyokuwa nayo, na kwa maana hiyo ulirudufu mtihani huo na matokeo yake nikayapata.¹⁸
2. Ibn Khuzaymah kama vile alivyokuwa Sheikh wa Bukhari na Muslim, kiistilahi anaitwa Sheikh wa Uislamu alikuwa na mwanafunzi wake aliyeitwa Muhammad bin Muumal anasema: Nilikuwa nikiongozana na mwalimu wangu Ibn Khuzaymah pamoja na Jumuiya ya watu tukienda kuzuru kaburi la Ali bin Musa Ridhaa [a.s] lililopo Tuus, mwalimu wangu Ibn Khuzaymah katika eneo lile alitabaruku na kupatukuza, aidha alinyenyekea na sisi tulinyenyekea pia.¹⁹

¹⁷ *Fat’hul Baari*, Juz. 2, uk. 557.

¹⁸ *Kitabu Thiqaat*, Juz. 8 uk. 456.

¹⁹ *Tahdhiib Tahdhiib*, Juz. 7, uk. 339.

Maswali na Majibu

3. Abu Ali Khilal Sheikh wa Hambali anasema: “Nilipopatwa na tati-zo nilikwenda kuzuru kaburi la Musa bin Ja’far [a.s] nilitawasuli kwake na Mwenyezi Mungu [a.j] alinitatulia tatizo langu.”²⁰
4. Muhammad bin Idris Shafii alikuwa anakwenda kufanya tawasuli katika kaburi la Abu Hanifa, na Ahmad bin Hambali alikwenda kwenye kaburi la Imam Shafii na kufanya tawasuli.²¹
5. Waislamu pindi walipopatwa na ukame walikwenda kwenye kaburi la Abu Ayub Answari kufanya tawasuli ili mvua inyeshe.²²
6. Ibn Khalkan na Dhahabi wote kwa pamoja wanasema: Watu walikwenda kuomba mvua na kufanya tawasuli kwenye kaburi la Ibn Fuuruk Isfahani aliyefariki mwaka 406 H ili mvua inyeshe.²³

Dondoo muhimu katika mchakato huu unaohusiana na ufanyaji tawassuli ni kwamba wanachuoni wakubwa wa Ahlu Sunna waliwahamasisha watu wazi wazi katika kuomba haja na kufanya tawassuli.

Qastwalaani anasema: Anastahili mwenye kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w] kuomba dua na kufanya tawassuli, vile vile aombe shufaa kupitia Bwana Mtume [s.a.w.w] bila shaka Mwenyezi Mungu ataitakabali shufaa ya Mtume [s.a.w.w] na mtu huyo atafanikiwa.²⁴

²⁰ *Tarekh Bahgdad*, Juz. 1, uk. 120.

²¹ *Manaqib Abi Hanifa*, Juz. 2, uk. 199.

²² *Mustadrak Hakim*, Juz. 3, uk. 518.

²³ *Wafayat Aayan*, Juz. 4, uk. 272, *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 17, uk. 215, Bukhari na watu wa Samarkand alieleza jambo hilo *Twabaqat Shafiiya*, Juz. 12 uk. 469 na *Twabaqat Shafiiyat*, Juz. 2, uk. 234.

²⁴ *Mawahib Laduniya*, Juz. 3, uk. 417.

Maswali na Majibu

Swali 6: Je! ipo dalili yoyote inayoruhusu kuzuru makaburi yaliyopo katika maeneo yetu?

Jibu: Katika kujibu Swali hilo tutaangalia aya za Qur’ani, Sunna ya Bwana Mtume [s.a.w.w] na matendo ya masahaba.

Qur’ani tukufu inasema: “Na lau wangelikuja kwako pindi walipodhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu Mwenye kupokea toba Mwenye kurehemu.”²⁵

Kwa hakika aya hiyo inahamasisha kumzuru Mtume [s.a.w.w] wakati akiwa hai na hata akiwa amefariki, hivyo hivyo Sabki anasema: Wanazuoni wote kwa ujumla waliitumia na kuitendea kazi aya hiyo wakati wa uhai wa Bwana Mtume [s.a.w.w] na pindi alipofariki, kwani zimepokewa hadithi chungu tele kutoka kwa Bwana Mtume [s.a.w.w] kuhusiana na suala hilo, Mtume [s.a.w.w] amesema: “Nikiwa hai ni heri kwenu mnazungumza na mimi, nami nazungumza nanyi, na nikiwa nimefariki aidha ni heri kwenu kwani amali zenu huonyeshwa kwangu...”²⁶

2. Sunna za Mtume [s.a.w.w]: Zipo hadithi nyingi sana zilizopokewa kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] ambazo zinashajiisha kuzuru kaburi lake tukufu baada ya kufariki kwake, baadhi ya hizo ni:

“Yeyote mwenye kuzuru kaburi langu lazima apate uombezi wangu.”²⁷

²⁵ Sura 4 aya 64.

²⁶ *Twarhul-Tathriib*, uk. 297.

²⁷ *Sunanul-Kubra*, Juz. 5, uk. 245

Maswali na Majibu

3. Matendo ya Masahaba:

Abdul-Razzaq Bahyaqi na Ibn Abdul-barri wamepokea kwamba Bi Fatimah Zahra [a.s] binti ya Mtume [s.a.w.w] kila Ijumaa alikuwa akienda kuzuru kaburi la ammi yake Seyyidina Hamza na huko alikuwa akisoma dua na kulia.

Hakim Naysaburi amesema: Mlolongo wa wapokezi wa hadithi hiyo ni unaohusisha watu waaminifu na wakweli.²⁸

Swali 7: Ipo hadithi inayosema: “Haifungwi safari isipokuwa kwenye misikiti mitatu.....” Je! hiyo sio dalili ya kuzuia kukusudia kuzuru makaburi?

Jibu: Tunajibu kama ifuatavyo:

1. Upo uwezekano kwamba kilichotengwa katika hadithi hiyo ni sehemu au msikiti, bali Qastwalaani²⁹ ameshadidia kwamba makusudio yake ni misikiti ndio ambayo hairuhusiwi kuifungia safari, kwa hivyo hakuna dalili yoyote ile ambayo inaharamisha kuzuru makaburi.
2. Kwa hakika hadithi yenyewe haizungumzii kabisa jambo hilo, ikiwa makusudio yake ni hayo basi haifai kwenda msikiti wowote isipokuwa misikiti hiyo mitatu... na hakuna shaka hilo lina kwenda kinyume na sunna ya Mtume [s.a.w.w] ambapo alikuwa kila jumamosi akienda kwenye msikiti wa Quba.

²⁸ *Muswanaf Abdul-Razzaq*, Juz. 3, uk. 572 – *Mustadrak Hakim*, Juz. 1, uk. 377 – *Sunan Kubra*, Juz. 4, uk. 131 – *Tamhiid Sherh Muwatwai*, Juz. 3, uk. 234 – na imepokewa kutoka kwa Khalifa wa pili Umar na Abdullah bin Umar amepokea hivyo pindi aliporejea kutoka safarini kwanza alikwenda kuzuru kaburi la Bwana Mtume [s.a.w.w], *Shifau Siqaam* uk. 44 na *Wafaul-Wafa*, Juz. 4 uk. 134...

²⁹ *Irshadu Saari*, Juz. 2, uk. 332.

Maswali na Majibu

3. Bilal Mhabeshi alifunga safari kutoka Sham hadi Madina ili kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w] na safari yake hiyo ilikuwa mashuhuri sana.

4. Wanachuoni wa makundi mawili [Shia na Sunni] walifunga safari ya kwenda kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w], kwa mantiki hiyo Ibn Taymiyya - ni mtu ambaye aliyeanzisha mzozo huo wa kuharamisha kuzuru makaburi - kwani alikemea vikali sana suala hilo.

Qastwalaani anasema: Kauli ya kukataza kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w] ni ya Ibn Taymiyya, nayo ni kati ya masuala ambayo yalimchukiza mno.³⁰

*Ghazali anasema: “Kila ambaye anamtabaruku Mtume [s.a.w.w] wakati akiwa hai basi amtabaruku baada ya kufariki kwake, aidha inaruhusiwa kufunga safari kwa lengo hilo.”³¹

5. Zipo hadithi zilizopokewa kutoka pande zote mbili ambazo zinashadidia juu ya mchakato huo wa kuzuru makaburi bila kuweka sharti lolote lile.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] amesema: “Nilikukatazeni kuzuru makaburi, basi hivi sasa zuruni.”³²

Ahlu Sunna wote wamefahamu ibara hiyo ambayo inasema: “Basi hivi sasa zuruni” ni ruhusa ya kufanya hivyo, bali Ibn Hazmi

³⁰ *Irshadu Saari*, Juz. 2, uk. 429.

³¹ *Ihyahul-Uluum*, Juz. 1, uk. 258 Dhahabi ana maoni katika utoleaji dalili wa hadithi hiyo, na *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 4 uk. 484.

³² *Sahih Muslim*, Juz. 3, uk. 65.

Maswali na Majibu

ameitikadi kuwa sio ruhusa tu bali ni wajibu kufanya hivyo.³³

Swali 8: Je! wanawake wanaruhusiwa kuzuru makaburi, ukizingatia imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] inayosema: “Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wanawake wenye kuzuru makaburi”?

Jibu: Jawabu la swali hilo ni kama ifuatavyo:

1. Ipo hadithi ambayo inaeleza kwamba “bi Fatimah Zahra [a.s] na bi Aisha walizuru makaburi, hakika Fatimah [a.s] alikuwa kila siku ya Ijumaa akizuru kaburi la ammi yake Hamza akiswali huko na kulia.”³⁴

Ibn Abi Maliika anasema: “Nilimuona Aisha akiwa juu ya kaburi la kaka yake Abdul-Rahman ambapo kaburi lake lipo Makka.”³⁵

2. Ama hadithi inayosema: “Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wanawake wenye kuzuru makaburi” ni hadithi iliyopokewa na Buruuda ambayo hukumu yake ilishafutwa, vile vile inapingana na zile ambazo huruhusu jambo hilo, kama ilivyoelezwa kinaga ubaga na Hakim Naysabuuri na Dhahabi kama ilivyokwisha tangulia hapo kabla.

Hadithi ya Buruda inasema: “Mtume [s.a.w.w] alikataza kuzuru makaburi, kisha akaamrisha kuyazuru.”³⁶

³³ *Taaju Jaamiu lil Usuul*, Juz. 1, uk. 381.

³⁴ *Sunanul-Kubra*, Juz. 4, uk. 132 na *Musanaf Abdul-Razzaq*, Juz. 3, uk. 572.

³⁵ *Muswanaf Abdul-Razzaq*, Juz. 3, uk. 570 na *Muujamul-Buldan*, Juz. 2, uk. 214.

³⁶ *Sunanul-Kubra*, Juz. 4, uk. 131 na *Mustadrak Hakim*, Juz. 1, uk. 374.

Maswali na Majibu

3. Wanazuoni wa Ahlu Sunna walitoa Fat'wa kwamba ni Sunna wanawake kuzuru makaburi.

*Ibn Abidiina anasema: Je! Wanawake wanaruhusiwa kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w]?

Jibu: Ndio, bila shaka wala karaha yoyote, kulingana na masharti yake kama walivyoeleza bayana baadhi ya wanazuoni suala hilo, ama kutokana na yale yaliyosihika na kukubaliwa na madhehebu yetu, na hayo ndiyo maneno ya Kurkhi na wengineo kwamba: Ruhusa ya kuzuru makaburi imethibiti kwa wanaume na wanawake kwa pamoja na jambo hilo halina mushkeli wala tatizo lolote, wapo wenye kusema ni sunna, bali wengine wamesema ni wajibu.³⁷

4. Hadithi hii “Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wanawake wenye kuzuru makaburi” Hadithi hiyo imepokewa kwa njia tatu, ambazo zote hizo ni dhaifu nazo ni:

Njia ya awali ya Ibn Khashiim ameeleza kwamba hadithi hizo sio hoja, hazina msingi wala sio za kutegemewa.³⁸

Njia ya pili ni ya Badhaani ambayo nayo haitegemewi wala haizingatiwi.³⁹

Ama njia ya tatu ya Umar bin Abu Salama ambayo vile vile ni dhaifu.⁴⁰

³⁷ Raddul-Muhtar, Juz. 2, uk. 263 na *Mawahibu Laduniya*, Juz. 3, uk. 405.

³⁸ *Miizanal Itidal*, Juz. 2, uk. 459.

³⁹ *Tahdhibul-Kamal*, Juz. 4, uk. 6.

⁴⁰ *Siyar Aalamu Nubalaa*, Juz. 6, uk. 33.

Maswali na Majibu

Swali 9: Je! kuna tatizo kuswali na kuomba dua pembezoni mwa kaburi la Mtume [s.a.w.w], mawalii na watu wema?

Jibu: Katika kujibu swali hilo tunasema:

1. Ipo aya tukufu inayosema: “Na lau wao wengelikuja pindi walipodhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyez Mungu ...” ni dalili inayojulisha ruhusa ya kuomba dua pembezoni mwa kaburi la Mtume (s.a.w.w) kwani Ibara: “wangelikuja” inahusu wakati wa uhai wake na baada ya kufariki kwake.

2. Fatimah Zahraa (a.s) alikuwa kila wiki akienda pembezoni mwa kaburi la Hamza na huko alikuwa akiomba dua na akilia. Hakika Naysabuuri anasema: Wapokezi wa hadithi hiyo wote ni waamini-fu na wakweli.⁴¹

3. Mwenendo wa waislamu kuhusiana na jambo hilo:

*Ibn Khalkan anasema: Sayyidah Nafii ambaye ni binti wa Hasan bin Zayd bin Hasan bin Ali bin Abi Twalib (a.s) aliyezikwa mahala panapoitwa “**Darbu Sibaya**” nchini Misri - palikuwa mashuhuri sana na ikawa ni sunna kuomba dua mahala hapo, pia lilikuwa ni jambo lililo mujarrabu sana.⁴²

*Imam Shafii mara kwa mara alikuwa akizuru kaburi la Abu Hanifa na hapo aliswali rakaa mbili.⁴³

*Zuhari alikuwa akiomba dua pembezoni mwa kaburi la Kurkhi naye amenukuu jambo hilo.⁴⁴

⁴¹ *Mustadrak Hakim*, Juz. 6, uk. 377.

⁴² *Wafayatul-Aayan*, Juz. 5, uk. 424.

⁴³ *Tarikh Baghdad*, Juz. 1, uk. 123.

⁴⁴ *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 9, uk. 343.

Maswali na Majibu

*Vivyo hivyo Jazli amenukuu kuhusiana na watu kuzuru kaburi la Imam Shaafi.⁴⁵

Swali 10: Je! ni nini makusudio ya hadithi inayosema: “Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi ambao wamefanya makaburi ya Mitume wao misikiti? na hadithi inayosema: “Ewe Mola wangu usifanye kaburi langu kuwa sanamu”?⁴⁶ Je! amekataza kuswali na kuomba dua pembezoni mwa kaburi lake hali kadhalika makaburi mengineyo?

Jibu: Aidha katika kujibu swali hilo kuna vidokezo kadhaa ambavyo inafaa kuvieleza kwanza kabla ya kujibu swali, baadhi ya hivyo ni:

1. Wapokezi wote wa hadithi hiyo ni dhaifu au hawajulikani, kwa mfano: “Abdul-Warith” ni mtu asiyekubalika kwa wanazuoni wa Ahlu Sunna, vivyo hivyo Abu Saleh ambaye haeleweki ni kati ya watu dhaifu au waaminifu, vile vile “Abdallah bin Uthman” hadithi ambayo yeye huipokea hutupiliwa mbali, ama “Ibn Bahaman” ni mtu asiyejulikana, kwa hivyo basi kuhusiana na mlolongo wa wapokezi wa hadithi hiyo una mushkeli na kwa mantiki hiyo hatuwezi kuifanyia kazi.
2. Kwa hakika hadithi hiyo haijulishi kabisa uharamu wa kuswali na kuomba dua pembezoni mwa makaburi, bali zipo baadhi ya hadithi ambazo zinaashiria kwamba Kanisa la Ethiopia lina utaratibu pindi anapokufa mmoja wa watu wao wema hujenga juu ya kaburi lake nyumba ya ibada, aidha picha zake hutundikwa humo, na watu husujudu kuelekea picha na kaburi lile, na hiyo ina maanisha kwamba hakuna uhusiano kati ya kumuabudu Mwenyezi Mungu [s.w.t] na kuswali sehemu yenye makaburi ya watu wema.

⁴⁵ *Jawahir Mudhiia*, Juz. 1, uk. 461.

⁴⁶ *Musnad Ahmad*, Juz. 2, uk. 246 na *Muwatwai*, Juz.1, uk. 172.

Maswali na Majibu

*Qurtubi anasema: Hakika wamechora picha za watu waliotangulia ili wapate kuwakumbuka hao na vitendo vyao vyema, na wanajitahidi kama walivyojitahidi hao, basi wakawa wanaabudu juu ya makaburi yao, kisha vikaja hapo baadaye vizazi vingine hawakujua makusudio yao, hapo shetani akawashawishi na kuwaghilibu kwamba wazee wao waliotangulia walikuwa wakiziabudu picha hizo na wakizitukuza, na Mtume (s.a.w.w.) alipokuja aliwatahadharisha kutokana na hayo.⁴⁷

*Baydhawi anasema: “Pindi Mayahudi na Manaswara walipokuwa wanasujudu juu ya makaburi ya Mitume yao kwa ajili ya kuwatukuza, kufanya Qibla chao na kuelekea wakati wa swala na yanayofanana na hayo wakayafanya kuwa masanamu, hapo wakalaaniwa na Mtume [s.a.w.w]...”⁴⁸

* Maelezo hayo hayana uhusiano wowote juu ya kuzuru kaburi la Mtume [s.a.w.w], Maimamu watakatifu na watu wema kwa lengo la kumuabudu Mwenyezi Mungu [a.j]

2. Wapo wanazuoni wengi wa Ahlu Sunna wametoa fat’wa ya kuruhusu kuswali pembezoni mwa makaburi, baadhi yao ni Malik bin Anas: “Maliki alikuwa haoni taabu kuswali katika makaburi, yeye alikuwa akiswali mbele ya kaburi, nyuma yake, kulia na kushoto kwake.”

Malik akasema: “Hakuna tatizo kuswali makaburini, na imenifikia habari kwamba masahaba wa Mtume [s.a.w.w] walikuwa wanaswali katika makaburi.”⁴⁹

⁴⁷ *Irshad Saari*, Juz. 3, uk. 497.

⁴⁸ *Irshad Saari*, Juz. 2, uk. 479.

⁴⁹ *Al Mudawwanatul-Kubra*, Juz. 1, uk. 90.

Maswali na Majibu

Abdul-Ghani Mnablusi anasema: “Iwapo msikiti utakuwa makaburi-ni au njiani, halafu mtu akakaa hapo au juu ya kaburi la walii wa Mwenyezi Mungu, mwanachuoni au mmoja wa watafiti kwa lengo la kuitukuza roho yake tukufu, ili kuwatangazia watu kwamba hapo amezikwa mmoja wa mawalii wa Mwenyezi Mungu [a.j] waweze kupata kutabaruku na kumuomba dua, bila shaka maombi yake yatakubaliwa, ni dhahiri hilo ni jambo zuri, lililoruhusiwa na wala halina kipingamizi chochote.....”⁵⁰

Swali 11: Je! ipo sheria inayokataza kujengea makaburi?

Jibu: Zipo hadithi kadhaa ambazo hukataza na zipo zenye kuruhusu suala hilo kama ifuatavyo:

1. Dalili ya kuharamisha jambo hilo ukiachilia mbali hadithi ya Abu Hayyaji hakuna hadithi nyingine ila hiyo pekee,⁵¹ aidha hadithi hiyo kuhusiana na mlolongo wa wapokezi wake una mushkeli, pamoja na kuwapo Wakii na Habiib bin Abu Thabiti ambao ni miongoni mwa wapokezi wa hadithi husika, kwani watu hao kwa mtanzamo wa Ahlu Sunna ni watu ambao wana utata.
2. Kuhusiana na dalili ya hadithi hiyo inahitajika kuchunguzwa vizuri kwani ibara inayosema: “Na wala kaburi isipokuwa nitali-sawazisha” haina maana kwamba yabomolewe majengo ya makaburi, bali ina maana lisiwekwe nundu juu ya kaburi, yaani kaburi lisiinuliwe sana kama vile nundu ya ngamia.

Qastwalaani anasema: “Kulisawazisha kaburi ni sunna, na haifai kuiacha sunna hiyo kwa kuitwa wasaliti, na hakuna tofauti baina ya kulisawazisha na hadithi ya Abu Hayyaji, kwani haikusudii kui-

⁵⁰ *Hadiiqatul-Nadiya*, Juz. 2, uk. 63.

⁵¹ *Sahihi Muslim*, Juz. 3, uk. 61.

Maswali na Majibu

sawazisha ardhi inayolizunguka kaburi, bali lengo lake kulisawazisha kaburi lenyewe...”⁵²

3. Mwenendo wa waislamu wa kila zama ulikuwa ni kujengea makaburi kama vile:

1. Kaburi la Mtume [s.a.w.w] lilijengewa kwa mawe.
2. Makaburi ya Maimamu yaliyopo Baqii yalikuwa yamejengewa, lakini mwaka 1345 Mawahabi walibomoa na kuvunja majengo yake.
3. Kaburi la Ibrahim ambaye ni mtoto wa Bwana Mtume [s.a.w.w] ambalo lilikuwa katika nyumba ya Muhammad bin Zayd bin Ali, na bila ajizi mawahabi walibomoa majengo yake na kuvunja vunjia.
4. Jengo la msikiti ambao ulikuwa katika kaburi la Hamza [a.s] mawahabi walilivunja mwanzoni mwa karne ya pili Hijiria.
5. Jengo la kaburi la Saad bin Maadhi, kaburi lake lilikuwa kwenye nyumba ya Ibn Aflaha na katika zama za kiongozi Umar bin Abdul-Aziz lilijengwa juu yake Quba.⁵³
6. Lipo jengo juu ya kaburi la Bahali ambalo lilijengwa mwaka 275 nchini Misri.⁵⁴
7. Lipo jengo juu ya kaburi la Amirul-Mu’minina Sayyidina Ali bin Abi Twalib [a.s] ambalo lipo Najaf nchini Iraq, ambalo lilijengwa karne ya pili Hijiria.⁵⁵

⁵² *Irshadu Saari*, Juz. 2, uk. 468.

⁵³ *Wafaul-Wafa*, Juz. 2, uk. 545.

⁵⁴ *Siyar Aalaamu Nubalaa*, Juz. 13, uk. 285.

⁵⁵ *Mausuatul-Utabat*, Juz. 6, uk. 97.

Maswali na Majibu

8. Kaburi la Salman Farsi limejengewa.⁵⁶

9. Lipo jengo katika kaburi la Abu Awaana ambalo lilijengwa mwaka 316 H.⁵⁷

Hitimisho, kwa hakika ni dhahiri shahiri kwamba mwenendo wa waislamu wawe Mashia pamoja na Masuni katika mchakato mzima wa suala la kuzuru makaburi ya viongozi wa dini pia watu wema, wao hujengea makaburi hayo, na wapo washika dau wengine ambao sio hujengea tu bali huzitukuza sehemu hizo, mwenendo huo ulikuwa ndiyo desturi na utamaduni katika miji yote ya Kiislamu na bado unaendelea hadi hivi sasa, kwa mfano makaburi ya Maimamu watukufu [a.s] yaliyopo Najaf, Kaadhimaini, Saamaraa, Mash'had na makaburi ya wanazuoni wakubwa wa Ahlu Sunna kama vile kaburi la Abu Hanifa na Abdul-Qaadir Jailani yaliyopo Baghdad na kaburi la Bukhari lililopo Samarkandi na mengineyo, huo ni ushahidi tosha juu ya yule ambaye anayekanusha jambo hilo, ni mawahabi pekee wa Hijazi [saudia] ndio ambao huenda kinyume na mwenendo huo.

Swali 12: Je! ni kweli Mtume [s.a.w.w] amekataza kuliweka kaburi katika mazingira mazuri, kulijengea?⁵⁸

Jibu: Mosi: Hadithi kama hizo zinatofautiana na mwenendo wa waislamu wote ambao umezoeleka na kuota mizizi, na jibu la swali hilo halina tofauti na majibu tuliyoaeleza katika suala lilitangulia.

Pili: Mlolongo wa wapokezi wa hadithi hiyo una utata ambao wahitajika kuchunguzwa, na miongoni mwa wapokezi wake yupo Abu Zubeir - ni Muhammad bin Muslim Amad - ambaye hakubaliki kabisa

⁵⁶ *Tarikh Baghdad*, Juz. 1, uk. 163.

⁵⁷ *Siyar Aalamu Nubalaa*, Juz. 14, uk. 419.

⁵⁸ *Sahihi Muslim*, Juz. 3, uk. 63.

Maswali na Majibu

na wanazuoni pamoja na wataalamu wa sifa na vigezo vya wapokezi wa hadithi, hali kadhalika wanachuoni wa hadithi wa Ahlu Sunna kama vile Ahmad bin Hambali, Ibn Uyaina, Shu'uba na Abu Hatam humuona ni mtu dhaifu na kwa hivyo hadithi iliyopokewa na yeye haifai kufanyiwa kazi.⁵⁹

Hivyo hivyo iwapo atakuwemo katika mlolongo wa wapokezi Hafswa bin Ghayathi, kwani huamini kuwa ni mtu dhaifu, kwa mantiki hiyo hawaikubali hadithi yake, vile vile Yakub bin Shayba ambaye ni mmoja kati ya wanachuoni wakubwa wa Ahlu Sunna hamkubali mtu huyo.⁶⁰

Vile vile katika mlolongo wa wapokezi wa hadithi hizo na zinazofanana na hizo wamo wapokezi ambao hawafai hata kidogo kusikilizwa maelezo na upokezi wao, kwa mfano Rabiia, Ibn Abu Shayba na Saaji.⁶¹

Hatimaye njia zote ambazo zimehusika kwa njia moja au nyingine upokezi wake zina mushkeli.⁶²

Swali 13: Je! inaruhusiwa kuwasha taa au mishumaa makaburini au hapana?

Jibu: Zipo dalili chungu nzima kuhusiana na kadhia hiyo, na tunajibu kama ifuatavyo:

⁵⁹ *Tahdhibul-Kamaal*, Juz. 26, uk. 407.

⁶⁰ *Tahdhibu-Tahdhiib*, Juz. 2, uk. 360, *Tarikh Baghdad*, Juz. 8, uk. 199 na *Siyar Aalamu Nubalaa*, Juz. 9, uk. 31

⁶¹ *Tahdhibu-Tahdhiib*, Juz. 9, uk. 143, *Miizanal-Iitidali*, Juz. 3, uk. 545 na *Tahdhibul-Kamaal*, Juz. 18, uk. 483.

⁶² *Al-Wahabiya*, dua wa Uruud, uk. 182.

Maswali na Majibu

1. Kulingana na hadithi sahihi za Bwana Mtume [s.a.w.w] ambazo zimepokewa na Wanachuoni wakubwa wa Ahlu Sunna ni kwamba Mtume [s.a.w.w] alipokuwa anataka kwenda makaburini usiku aliamrisha ziwashwe taa.⁶³
2. Mwenendo, desturi na utamaduni wa waislamu ulikuwa ni huo, na hata baadhi ya masahaba na watu wema pia walikuwa wakiwasha kandili makaburini.

Historia inaeleza kwamba kaburi la Abu Ayub Answare katika karne ya nne liliwekwa kandili.⁶⁴

* Katika karne hiyo ya nne juu ya kaburi la Zubeir bin Awam iliwekwa kandili.⁶⁵

* Vile vile katika kaburi la Imam Musa bin Ja'far [a.s] mwanzoni mwa karne ya tano liliwashwa kandili na kuachwa mahala hapo.⁶⁶

3. Ama hadithi inayosema: “Mwenyezi Mungu anawalaani wale ambao wanajenga misikiti makaburini na kuweka taa” sanadi na mlongo wa wapokezi wa hadithi hiyo una mushkeli, na mpokezi wa hadithi hiyo ni Abu Swaleh ambaye kwa mtazamo wa Ahlu Sunna ni mtu dhaifu na asiyekubalika, ama maelezo ya hadithi hiyo, imeelezwa kwamba katazo la hapo ni la muongozo na ushauri, na sio katazo ambalo iwapo mhusika wake akienda kinyume nalo hupata dhambi, hayo yameelezwa na Sindi, Azizi, Ali Naswif na Sheikh wa Hanafi.⁶⁷

⁶³ *Jaamiu Sahihi*, Juz. 3, uk. 372.

⁶⁴ *Tarikh Baghdad*, Juz. 1, uk. 154.

⁶⁵ *Al-Muntadham*, Juz. 14, uk. 383.

⁶⁶ *Wafayat Aayan*, Juz. 5, uk. 310.

⁶⁷ *Shereh Jamiu Swagiir* Juz. 3, uk. 198, *Sunan Nasai* Juz. 4, uk. 95, *Taaju* Juz. 1, uk. 381.

Maswali na Majibu

Swali 14: Je! inafaa kuweka nadhiri juu ya watu wema, waumini na waliofariki?

Jibu: Ndio, iwapo itawekwa nadhiri kwa Mwenyezi Mungu [a.j] na kukusudia thawabu yake iwafikie hao, jambo hilo limeenea kwa wafuasi wa Ahlul Bayt na halina tatizo kama ifuatavyo:

1. Zipo hadithi ambazo zinapatikana katika vitabu vya Ahlu Sunna zinazoelezea na kuruhusu jambo hilo, imepokewa hadithi kutoka kwa Thabiti bin Dhahak kutoka kwa Mtume [s.a.w.w] kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume [s.a.w.w] hivi: Kuna mtu ameweka nadhiri na amechinja kwa lengo la Bawanah? Mtume [s.a.w.w] akasema: Je! Bawanah alikuwa hapo kabla ni miongoni mwa masanamu yaliyokuwa yakiabudiwa? Wakasema: Hapana, akauliza: Je! ilikuwa katika iddi zao? Wakasema: Hapana, Mtume [s.a.w.w] akasema:

“Atekeleze nadhiri yake kwani nadhiri haitekelezwi katika mambo ya haramu ambayo yanamuasi Mwenyezi Mungu [s.w.t], wala katika mambo ambayo mwanadamu hayamiliki.”⁶⁸

Kwa hivyo ikiwa nadhiri itahusiana na mila za kijahilia, yaani kuhusu masanamu na iddi za makafiri nadhiri hizo kutekeleza sio lazima hata kama wapo baadhi ya wale wanaowafuata Ahlul-Bayt ambao hupendelea sharti la nadhiri kujikurubisha katika mahala imetiliwa mkazo, hilo halina msingi na lenye kupuuzwa, ala kuli hali Ahlu Sunna huzipokea hadithi hizo na zinazofanana na hizo aidha huzinukuu, kwani zinaelezea bayana kufaa na kuruhusiwa kuweka nadhiri katika sehemu hizo tukufu, na kutoa zawadi kwa ajili ya watu wema na wau-mini.

⁶⁸ *Sunan Abu Daud*, Juz. 3, uk. 238.

Maswali na Majibu

2. Katika kutilia mkazo zaidi juu ya suala hilo Izaami Shafii anasema: Mtu anayeweza kuweka nadhiri kwa waislamu inatimia, vivyo hivyo akikusudia kuchinja na kuweka nadhiri ya kutoa zawadi kwa ajili ya waliokufa na thawabu zake ziwafikie wao ni jambo zuri linalofaa na wala halina ubaya wowote ule, kwani Ijimaa [kongamano] la Ahlu Sunna linaunga mkono watu waliohai kuwapa swadaka wale waliokufa, zipo hadithi chungu tele zinazoelezea hilo, kama inavyotoa ishara hadithi ifuatayo:

Imepokewa kutoka kwa Saad kwamba siku moja bwana mmoja alimuuliza Mtume [s.a.w.w]: Mama yangu amefariki na yakini ninayo kwamba kama angelikuwa hai ningemtolea swadaka na thawabu yake ingelimfikia, Je! nikitoa swadaka ili thawabu yake imfikie itamfikia? Mtukufu Mtume [s.a.w.w] akasema: “Ndio” akauliza tena: je! ni swadaka ipi ambayo inafaa zaidi? Akasema [s.a.w.w]: “Maji” basi Saad akachimba kisima cha maji akajaalia kuwa ni swadaka na thawabu zake zimfikie mama yake.⁶⁹

3. Yapo makaburi mengi ya waislamu sehemu mbali mbali kati ya hayo manane yalijulikana kama makaburi ya nadhiri ambayo walikuwa waislamu wakiweka nadhiri katika makaburi hayo, kama vile:

- Kaburi la Bustii lililopo nchini Morocco.
- Kaburi la nadhiri lililopo Baghdad.
- Kaburi la Ahmad Badawi n.k.⁷⁰

Swali 15: Je! Uislamu unaruhusu kufanya sherehe na maombolezo au hapana?

⁶⁹ *Furaanul-Qur'an*, uk. 133.

⁷⁰ *Naylu Ibtihaj*, Juz. 2, uk. 62, *Mawahib Laduniya*, Juz. 5, uk. 346 na *Tarikh Baghdad*, Juz. 1, uk. 123.

Maswali na Majibu

Jibu: Bila shaka na kwa yakini kabisa jambo hilo linaruhusiwa kama ifuatavyo:

1. Kuna kanuni ya kisheria inayosema: Vitu vyote vilivyopo duniani asili yake ni hufaa na vimeruhusiwa, isipokuwa itakapopatikana dalili ambayo inasema kinyume na hivyo.
2. Zipo aya za Qur'ani ambazo zinahamasisha kuadhimisha na kuhimiza zitukuzwe alama za dini, na hilo huzingatiwa ni katika uchamungu wa roho n.k.
3. Huo ndio mwenendo, desturi na utamaduni wa waislamu waliotangulia hapo kabla na hadi wa hivi leo, bali kuna thawabu nyingi katika kuadhimisha na kusherehekea mazazi ya Bwana Mtume [s.a.w.w], kama vile Qastwalaani na Diyar Bakr walivyoliashiria jambo hilo.⁷¹
4. Ni Mwenendo wa waislamu Mashia na Masunni wa kuweka vikao mbali mbali vya maombolezo na matanga kuhusiana na wale waliotangulia mbele ya haki. Hivyo hivyo Dhahabi alifanya hivyo katika kifo cha Jawiini aliyekufa mwaka 478 H, anaandika hivi: Masoko yalifungwa na waombolezaji wakaomboleza, na miongoni mwao ilikuwa idadi kubwa ya watoto ambao imekadiriwa kufikia mia nne, waliondoa vitambaa vichwani mwao na wakafanya hivyo kwa muda wa mwaka mzima, wanafunzi wakawa wanapita njiani wakiimba nyimbo za huzuni.⁷²

Kuhusu kusindikiza jeneza, Abdul-Muumini aliyefariki mwaka 346 H anaandika katika kitabu chake hivi: "Tulikeshwa tukisikia sauti za

⁷¹ *Tarikh Khamiis*, Juz. 1, uk. 323 na *Mawahib Laduniya*, Juz. 1, uk. 27.

⁷² *Siyar Aalamu Nubalaa*, Juz. 15, uk. 481.

Maswali na Majibu

ngoma za maombolezo, hadi ikafikia baadhi yetu kudhani kwamba jeshi limeingia.”⁷³

Ama kuhusu pindi unapotokea msiba, Ibn Jauzi aliyefariki mwaka 597H anaandika: “Na wakalala matanga pembezoni mwa kaburi lake kwa muda wote wa mwezi wa Ramadhani wakiomboleza na kuweka matanga na kuwasha mishumaa na kandili.... Basi tukaomboleza hadi asubuhi ya Jumamosi, hapo nikazungumza na kwa hakika watu wengi walihudhuria, kisha ikagaiwa mirathi...”⁷⁴

Swali 16: Je! ndoa ya Mut’aa ipo na imekubaliwa na wanachuoni wakubwa wa Ahlu Sunna?

Jibu: Ndio, kutokana na vidokezo vifuatavyo:

1. Ibn Jureji Umawi Sheikh wa Bukhari ambaye Ahlu Sunna wamemnasibisha kuwa ni miongoni mwa waaminifu na wakweli, amekubalika kwa maoni ya wanaij’maa, aidha vitabu sahihi vyote sita kwa pamoja vimenukuu hadithi ambazo zimepokewa na mwanachuoni huyo, imethibiti kwamba alioa ndoa ya muda zaidi ya wanawake 70.

Dhahabi anasema: Yeye ni mmoja wa wanachuoni wakubwa waaminifu... na kwake ndoa ya Muta’a ilikuwa ni jambo la kawaida kwani alioa wanawake wasiopungua 70 kwa ndoa ya muda, naye alikuwa anaona ni miongoni mwa mambo yaliyoruhusiwa kisheria, na alikuwa ni Faqih na mwanachuoni wa sheria katika mji wa Makka katika zama zake.⁷⁵

⁷³ *Siyar Aalamu Nubalaa*, Juz. 15, uk. 379.

⁷⁴ *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 18, uk. 379.

⁷⁵ *Miizanal-Itidal*, Juz. 2, uk. 659 na *Tahdhiib Tahdhiib* Juz. 6, uk. 360.

Maswali na Majibu

2. Masahaba wakubwa kama vile Abdullah bin Abbas, Jaabir bin Abdillah Answari, Imrani bin Haswiin, Abu Sa'id Khudri na Amiiirul-Mu'miniina Ali bin Abi Twalib [a.s] walifunga ndoa hiyo.
3. Umar bin Khatwab alisema wazi wazi: "Mambo mawili yalikuwako katika zama za Mtume [s.a.w.w] mimi nayaharamisha, aidha natoa adhabu kwa atakayeyafanya" moja kati ya hayo ni ndoa ya Muta'a.
4. Hivyo hivyo Qawshaji katika kitabu chake *Sherhu-Tajriid* uk. 484, ibara hiyo aliieleza na kuipinga!
5. Katika kitabu *Tarikh Twabari*⁷⁶ lipo katazo hilo la Umar, Imran bin Sawad yeye binafsi jambo hilo lilimuuma sana, vile vile watu wengi walimpinga Umar kutokana na ukatazaji wake wa ndoa ya muta'a, na yamesemwa mengi kuhusiana na yeye.
6. Umar bin Khatwab yeye mwenyewe hakusema kwamba Mtume [s.a.w.w] alikataza au kuiharamisha, bali alisema: "Mimi nai-haramisha..."
7. Kuna hadithi moja tu ambayo inasema kwamba Mtume [s.a.w.w] aliharamisha ndoa ya muta'a, na hadithi hiyo haijulikani wala hata haijatajwa na kitabu chachote katika vitabu vya wapokezi wa hadithi na wala hawakuipokea.
8. Ipo aya katika Qur'ani tukufu ambayo inaelezea suala hilo, na ime-thibiti kwamba hakuna aya nyingine iliyokuja kufuta hukumu hiyo.
9. Hali kadhalika Amirul-Mu'miniina Ali bin Abi Twalib [a.s]

⁷⁶ *Tarikh Twabari*, Juz. 2, uk. 579.

Maswali na Majibu

alinukuliwa akisema: “Lau Umar asingeliiharamisha ndoa ya muta’a asingezini ila mtu muovu sana.”

Swali 17: Je! kwa nini Mashia wanaposwali hawafungi mikono?

Jibu: Mashia huharamisha hilo, hata Masunni au madhehebu ya Ahlu Sunna hawasemi kuwa ni wajibu bali ni jambo la sunna, na wapo baadhi yao wanaoona ni wajibu kufanya hivyo, na miongoni mwao wapo wanaoona ni makuruhu kama vile kiongozi wa madhehebu ya Malik, yeye anaona kufunga mikono katika swala ni makuruhu na ni dhahiri kuwa masahaba wote walipokuwa wanaswali waliachia mikono hadi pale Umar alipoanzisha bidaa hiyo, hayo yamesemwa na baadhi ya masahaba kama vile Abdullah bin Zubeir, Hasan Baswari, Ibn Siirin, na miongoni mwa tabiina [kizazi hilichokuja baada ya masahaba] kwa mfano Hayath bin Saad na Ibrahim na Nakhai.

2. Mtume [s.a.w.w] hakuwali hivyo, Qurtubi anasema: “Wanazuoni wamehitilafiana kuhusu kuweka mkono mmoja juu ya mwingine katika swala, Imam Malik aliona ni makuruhu katika swala ya sunna na aliruhusu katika swala ya faradhi, na kuna baadhi ya Ahlu Sunna wanaoona kuwa kufunga mikono katika swala ni sunna, na sababu ya kutofautiana kwao ni kutokana na maelezo yaliyokuja juu ya namna ilivyokuwa swala ya Mtume [s.a.w.w], na wala haikupokewa kutoka kwao kwamba Bwana Mtume [s.a.w.w] aliweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto na walikuwa wakiamrishana kufanya hivyo.”⁷⁷

3. Ahlu Sunna wanategemea dalili ya hadithi ya Bukhari na Muslim: *Hadithi ya Bukhari: Imepokewa kutoka kwa Abu Hazim kutoka kwa Sahal bin Saad amesema: Walikuwa watu wakimuamrisha mtu

⁷⁷ *Bidayatul-Mujtahid*, Juz. 1, uk. 136.

Maswali na Majibu

mmoja kuweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika swala, Abn Hazim anasema: Sijui jambo hilo kama liliamrishwa na Mtume [s.a.w.w].⁷⁸

DONDOO:

Hajulikani ni mtu gani ambaye watu walimlazimisha kufanya hivyo Je! alikuwa ni Umar au mtu mwingine? Vivyo hivyo kutoka kwa Ayni ambaye amesherehesha *Sahih Bukhari* amesema: Hadithi hiyo ni mursal ambayo [haina wapokezi],⁷⁹ na vivyo hivyo imepokewa kutoka kwa Suyutwi.⁸⁰

*Kutoka kwa Alqama bin Wail na mtumishi wao: Hakika Wail bin Hajar alimwona Mtume [s.a.w.w] akiunyanyua mkono wake alipoingia katika swala... kisha akaweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto,⁸¹ hali kadhalika hadithi hiyo ni mursal ambayo haina wapokezi, na Ahlu Sunna wameikubali hadithi hiyo ambayo wamekiri kuwa hadithi ya Alqama ni mursal.

Ibn Hajar amepokea kutoka kwa Ibn Muiin amenukuu hivi: Alqama bin Wail kutoka kwa baba yake amesema ni hadithi mursal.⁸²

4. Ahlul-Bayt wa Mtume [s.a.w.w] walikemea na kukataza kufanya hivyo kwa ibara: “Usifunge mikono katika swala” na mahala pengine walisema: “Majusi [waabudu moto] ndiyo waliokuwa wakifanya hivyo.....” kwa hivyo walizuia kabisa jambo hilo, na

⁷⁸ *Sahih Bukhari*, Juz. 1, uk. 135.

⁷⁹ *Umdatul-Qaari*, Juz. 5, uk. 278.

⁸⁰ *Tawshiih ala Jaamiis-Sahih*, Juz. 1, uk. 463 na *Naylul-Autwar*, Juz. 2, uk. 187.

⁸¹ *Sahih Muslim*, Juz. 1, uk. 150.

⁸² *Tahdhiib Tahdhiib*, Juz. 7, uk. 247 na *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 13, uk. 193.

Maswali na Majibu

imeelezwa na baadhi ya vianzo na rejea vya kuaminika kwamba asili ya kitendo hicho ni Waajemi ndiyo ambao walimfanyia Khalifa wa pili Umar bin Khatwab naye akaamrisha watu wafanye hivyo katika swala.⁸³

Swali 18: Swala ya tarawehe ni ipi, na kwa nini Ahlu Sunna wanaidumisha?

Jibu: Kwa hakika asili ya swala za sunna za usiku katika mwezi wa Ramadhani ni rakaa ishirini au thelathini, na hadi hapo hakuna ikhtilafu yoyote katika makundi ya waislamu, lakini tofauti inapatikana kuswaliwa jamaa, kulingana na alivyonukuu Bukhari imepokewa kutoka kwa Umar bin Khatwab kwamba yeye ndiye ambaye aliye-wataka watu waswali kwa jamaa na akaiita hiyo ni bidaa nzuri:

Umar akasema: Hakika mimi naona ni vizuri lau watakusanywa na kisha wakaongozwa na msomaji mmoja, akafanya hivyo na Ubay bin Ka'b akamfanya kuwa Imam, usiku uliofuata akatoka nje ya nyumba yake basi akawaona watu wakiongozwa na Imam katika swala ya tarawehe, hapo akasema: "Bidaa nzuri iliyoje hii..."⁸⁴

Qastwalaani anasema: Umar anaeleza hapo wazi wazi kwa ibara ya "bidaa" ambayo ameanzisha, kwa sababu Mtukufu Mtume [s.a.w.w] hakuwaambia watu waswali swala ya tarawehe kwa jamaa, aidha haikuswaliwa jamaa katika zama za Abu Bakr.⁸⁵

Na Ayni anasema: Ama kulingana na ibara ya Umar kwamba ameanzisha "bidaa" hiyo ni dalili tosha inayojulisha Bwana Mtume

⁸³ *Jawahirul-Kalaam*, Juz. 11, uk. 19 na *Misbahul-Faqiiah*, uk. 402.

⁸⁴ *Sahih Bukhari*, Juz. 1, uk. 342.

⁸⁵ *Irshadu Saari*, Juz. 4, uk. 656.

Maswali na Majibu

[s.a.w.w] hakuwaambia watu waswali kwa jamaa, na hivyo hivyo haikuwa wakati wa Khalifa wa kwanza Abu Bakr.⁸⁶

Hali kadhalika Qulgushndi anasema: Umar ni mtu wa kwanza aliye-fanya sunna ya Ramadhani kuwa jamaa, na hilo alilifanya katika mwaka wa 14H.⁸⁷

Swali 19: Je! ni kweli bidaa imegawanyika sehemu mbili bidaa nzuri na bidaa mbaya? kwa mtazamo wa Khalifa wa pili ni ipi bidaa nzuri?

Jibu: Muislamu huona kuwa bidaa yoyote ile ni upotovu, imekuja katika hadithi kwamba: “Kila bidaa ni upotovu na kila upotovu ni motoni,” kwa hivyo bidaa kuigawanya kuwa ni bidaa nzuri na bidaa mbaya bila shaka hilo halikubaliki na wanazuoni wakubwa wa Ahlu Sunna, kwani wao suala hilo hulikemea vikali mno, kwa mfano bwana Shatwibi, Ibn Rajab Hambali na Thamidi kutoka kwa waandishi wa zama hii wa Saudia katika kitabu kiitwacho: “*Haqiqatul-Bidaa wa Ahkamuha*” imeadikwa hivi: Kauli inayosema kuwa kuna baadhi ya bidaa ni nzuri hilo linapingana na dalili za kisheria ambazo zinakemea na kulaumu bidaa ya aina yoyote ile, bali zipo hadithi zinazolaani vikali bidaa na kutahadharisha moja kwa moja jambo hilo, na hadithi zilizo nyingi hazitengi kwamba zipo bidaa nzuri ambazo zinakubalika mbele ya Mwenyezi Mungu [a.j]... na kanuni inayotumika kukataza bidaa ni kanuni hiyo ambayo inahusisha na kujumuisha mambo yote na kwa watu wote wala haitengi na kuwatoa baadhi ya watu na kuwaacha wengine au kuwaruhusu waanzishe bidaa wazitakazo....⁸⁸

⁸⁶ *Umdatul-Qaari*, Juz. 11, uk. 126.

⁸⁷ *Maathar Inafat fi Maalim Khilafa*, Juz. 2, uk. 337.

⁸⁸ *Haqiqatul-Bid'a wa Ahkamuha*, Juz. 1, uk. 138.

Maswali na Majibu

Swali 20: Zimepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu’miniina Ali bin Abi Twalib [a.s] kwamba aliswali swala ya tarawehe au alianisha Imam wa jamaa au alisema: “Mwenyezi Mungu atie nuru kaburi lake kama alivyotia nuru misikiti yetu,... Je! Vipi hukusanyika pamoja hadithi hizo na zile ambazo zinaelezea kwamba “ni bidaa tarawehe kuswaliwa jamaa?”

Jibu: Kwa hakika hadithi hizo na zinazofanana na hizo kwa mtazamo wa Shi’ah ni uzushi wa dhahiri, vile vile kutokana na mtazamo wa wanachuoni wa Ahlu Sunna wamethibitisha kwamba sio hivyo, na hivyo hivyo katika mchakato wa kukanusha hilo mwanachuoni Bayhaqi amenukuu hadithi nne au tano ambazo yeye mwenyewe amekiri kwamba sanad au upokezi wake ni dhaifu, na utafiti wowote utakaofanywa juu ya sanad yake itathibiti kwamba hilo sio sahihi.

Na kuongezea zaidi juu ya hilo tunasema: Haijathibiti katika historia kwamba Umar bin Khatwab binafsi aliswali swala ya tarawehe kwa jamaa! vile vile imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Umar ambaye ni mtoto wa Umar bin Khatwab aliikataza na kuikemea vikali swala ya tarawehe kuswaliwa jamaa.

Hali kadhalika Amirul-Mu’miniina Ali bin Abi Twalib [a.s] wakati wa ukhalifa wake alipokuwa mji wa Kufa nchini Iraq aliipinga, aliikemea na kuikataza.

Pindi alipokuwa Amirul-Mu’miniina Ali bin Abi Twalib [a.s] huko Kufa walimjia watu na kumwambia: Tuwekee imamu atuswalishe swala ya usiku wa mwezi wa Ramadhani, akawaambia: Hapana, hakuwakataza kukusanyika hapo, na ilipofika jioni wakawa wanawaambia watu: “Ieni Ramadhani ee Ramadhani sunna ya Umar.”⁸⁹

⁸⁹ *Sarair*, Juz. 3, uk. 639.

Maswali na Majibu

Swali 21: Je! tangu mwanzo wa kuruhusiwa adhana ilikuwepo ibara isemayo: “*Asswalatu khairu minan nawm*” au iliongezwa hapo baadaye?

Jibu: Kutokana na dalili zitakazofuata itadhihirika kwamba ibara hiyo haikuwa sehemu ya dhana:

1. Ipo hadithi sahihi ambayo imepokewa na Ahlu Sunna, ni hadithi iliyopokewa na Muhammad bin Is’haq amesema: “Ibara *Asswalatu khairu minan naum* haikuwepo.”⁹⁰
2. Saad bin Mujiib anasema kinaga ubaga kwamba: “Ibara hiyo iliingizwa katika adhana ya swala ya alfajiri baadaye.”⁹¹
3. Imam Malik katika kitabu chake “*Muwatwai*” amesema wazi wazi kwamba: Umar bin Khatwab ndiye aliyeamrisha iwekwe ibara hiyo katika swala ya asubuhi.

Kutoka kwa Malik amesema kinaga ubaga kwamba mwadhini alikwenda kwa Umar bin Khatwaab kumwamsha kwa ajili ya swala ya asubuhi, akamkuta bado angali analala hapo akasema: “*Asswalatu khairu minan-naum*” Umar akaamrisha iwekwe katika adhana ya asubuhi.⁹²

4. Imam Shafi’i anaona jambo hilo ni makuruhu, vile vile anaona ni bidaa, lakini hajui ni bidaa gani kati ya bidaa mbili, vile vile Shawkani anasema: “Na kama ibara hiyo ingelikuwako katika adhana tangu mwanzoni wala asingeikanusha Sayyidina Ali bin Abi Twalib [a.s], mtoto wa Umar bin Khatwab na Tausi.”⁹³

⁹⁰ *Naylu Autwar*, Juz. 2, uk. 37.

⁹¹ *Naylu Autwar*, Juz. 2, uk. 37.

⁹² *Muwatwai*, Juz. 1, uk. 72.

⁹³ *Naylu Autwar*, Juz. 2, uk. 38.

Maswali na Majibu

5. Ibn Jureji amepokea kutoka kwa Umar bin Hafswa amenukuu kwamba Saad ndiye mtu wa mwanzo ambaye alisema katika adhana ibara hii: “*Asswalatu khairun minan naum*” wakati wa ukhalifa wa Umar bin Kwatwab.⁹⁴
6. Aidha Ibn Naim anasema: Wala hatusemi katika adhana ibara hii: “*Asswalatu khairun minan naum*” kwa sababu haikuletwa na Bwana Mtume [s.a.w.w].⁹⁵

Swali 22: Je! Ibara “*Hayya’ala kharil a’mal*” ni maneno ya adhana? Na je! yupo yeyote miongoni mwa masahaba au kizazi kilichokuja baadaye aliyeadhini na kusema maneno hayo?

Jibu: Kulingana na hadithi sahihi zilizopokewa kutoka kwa mtoto wa Umar bin Khatwab na Abu Amama bin Sahal bin Haniif, watu hao – pamoja na kuondolewa maneno hayo katika adhana – lakini wao waliendelea kuyasema katika adhana.⁹⁶

Vile vile Bayhqi amepokea hadithi kutoka kwa Imam Zaynul-Abidiina [a.s] amenukuu kwamba mheshimiwa huyo aliyaweka maneno hayo katika adhana na akasema: Maneno hayo yalikuwepo katika adhana ya awali.⁹⁷

Vivyo vivyo Hasan bin Yahya bin Ju’ud, Zayd bin Arqam na Imam Shafi’i – katika moja ya kauli zake mbili – ibara hiyo wameitaja.⁹⁸

⁹⁴ *Muswanaf Abdul-Razzaq*, Juz. 1, uk. 474.

⁹⁵ *Muhala*, Juz. 3, uk. 160.

⁹⁶ *Muhala*, Juz. 3, uk. 160.

⁹⁷ *Sunanul-Kubra*, Juz. 1, uk. 624.

⁹⁸ *Naylul-Autwar*, Juz. 2, uk. 39, bila shaka jambo hilo ni kitendawili kwa mtazamo wa Ahlu Sunna.

Maswali na Majibu

Swali 23: Ni upi mtazamo sahihi kuhusu rajaa?

Jibu: Katika kuliweka wazi suala la rajaa husemwa hivi:

- i. Makusudio ya rajaa ni kurejea baadhi ya waumini na makafiri hapa duniani baada ya kufa, zama za kudhihiri Imam na kiongozi wa zama hizi [a.f], na jambo hilo sio muhali na lisilowezekana, bali ni jambo ambalo limethibitishwa na hadithi nyingi sana, na kwa mantiki hiyo hakuna tatizo lolote litakalopatikana kuhusiana na itikadi hiyo, lakini wapo baadhi ya Ahlu Sunna ambao hulikanusha hilo na hawalikubali.
- ii. Kwa hakika ipo mifano mbali mbali kuhusiana na suala la rajaa katika umma na jamii zilizotangulia hapo kabla, kama vile:
 - a. Kurejea hai watu 70 wanaotokana na kaumu ya Nabii Musa [a.s].
 - b. Kurejea hai maelfu ya watu baada ya kufa, Qur'ani tukufu inasema: Je! Hujui wale ambao walitoka makaburini na wakaishi tena ...⁹⁹
 - c. Kujerea na kuishi tena Uzair katika uhai wa kawaida baada ya kuwa mfu kwa muda wa miaka mia moja, Qur'ani tukufu inasema: **“Au kama yule ambaye aliyepita katika kijiji nacho kimeangukiana na sakafu zake, akasema: Mwenyezi Mungu atakiuhishaje [kijiji] baada ya kufa kwake? Basi Mwenyezi Mungu akamuua miaka mia, kisha akamfufua...”**¹⁰⁰
 - d. Kurejea hapa duniani na kuishi tena Saam bin Nuhu.
 - e. Kurejea watoto wa Nabii Yakub [a.s] na kuishi hai tena.¹⁰¹
 - f. Kurejea Yushaa, Ilyasa na Ishmuil na kuishi hai tena.¹⁰²

⁹⁹ Sura 2 aya 243.

¹⁰⁰ Sura 2 aya 259.

¹⁰¹ *Durrul-Manthuur*, Juz. 5, uk. 316, *Jaamiul-Bayaan*, Juz. 16, uk. 42, *Tafsir Nayshaburi*, uk. 44, *Shi'ah Waraja'a*, Juz. 2, uk. 154 na *Raja'at az nadhare Shi'ie* uk. 28.

¹⁰² *Tarikh Twabari*, Juz. 1, uk. 280, *Mukhtasar Twabari Tarikh Damascus*, Juz. 11, uk 170 na *Al-Kaamil fi Tarikh*, Juz. 1, uk. 154.

Maswali na Majibu

iii. Vile vile katika umma huu wa kiislamu tunayo mifano hai mingi ya kurejea watu na kuishi tena hapa duniani baada ya kufa, kwa mfano Ibn Abi Dunia ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanazuoni wakubwa wa Ahlu Sunna aliyekufa mwaka 208 H.

Kwa hivyo kuhusiana na mada hiyo kimeandikwa kitabu ambacho kimepewa jina: “*Man A’asha ba’adal Mauti*” [aliyeishi baada ya kufa], kitabu hicho kimechapishwa Saudia, hivi sasa kimetarjumiwa katika lunga ya kiajemi kinaitwa: “*Nemuunehaye Az Kasaanikera ke Ba’ada az Marghe zende shodeeand,*” na nakala zake zipo kwa watu hadi hivi sasa, baadhi ya mifano ya watu ambao walikufa kisha wakaishi tena ni:

1. Kurejea Zayd bin Kharija na kuishi tena baada ya kufa.
2. Kurejea kijana anayetokana na Answari na kuishi tena baada ya kufa.
3. Kurejea mtu miongoni mwa watu ambao waliuawa na Musaylamah na kuishi tena baada ya kufa.
4. Kurejea Ibn Kharash na kuishi tena baada ya kufa.
5. Kurejea mmoja wa waabudu masanamu – Daayi – Ibn Dhahak na kuishi tena baada yakufa
6. Kurejea Ruuban bint Bayjun na kuishi tena baada ya kufa.
7. Kurejea mtu kutoka ukoo wa Bani Juhaynah na kuishi tena baada ya kufa na mifano mingineyo.

Hali kadhalika imepokewa hadithi kutoka kwa Bwana Mtume [s.a.w.w] amesema: “Yatatokea katika umma wangu yale yaliyo tokea

Maswali na Majibu

kwa Bani Israil moja baada ya lingine.”¹⁰³

Bukhari anasema: Imepokewa hadithi kutoka kwa Bwana Mtume [s.a.w.w] amesema:

“Hakika mtafuata nyendo za wale waliokuwa kabla yenu shibri baada ya shibri na dhira baada ya dhira hata walipoingia katika shimo la kenge mtawafuata,” masahaba wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni Mayahudi na Manaswara? Akasema: “Ndio hao, mnadhani nawakusudia wengine?”¹⁰⁴

Hitimisho:

Kwa hivyo kutokana na mchakato huu wa kubainisha uhakika wa rajaa, imepokewa hadithi kutoka kwa Maimamu watoharifu zisizopungua mia tano ambazo zinaelezea kadhia hiyo, achilia mbali aya chungu nzima za Qur’ani tukufu ambazo tafsiri yake imeweka bayana suala la hilo.¹⁰⁵

Allama Twabatwabai ambaye ni mwanachuoni mashuhuri na mfasiri mkubwa wa Kishia kuhusiana na rajaa anasema: “Ikiwa suala hili limeeleweka, basi zipo aya nyingi ambazo Maimamu watoharifu [a.s] wameeleza kwamba: Maimamu watarejea na kuishi tena kabla ya Kiyama baada ya kudhihiri Imam wa zama hizi, bila shaka limefahamika hilo kulingana na vidokezo na dondoo tatu tulizozieleza, lakini wapo watu ambao hawajafanya utafiti juu ya ukweli na uhakika wa Kiyama, na katika kulieleza vizuri suala hilo inaweza ikawapambanukia hakika na unyeti wa siku hiyo, na kwamba maana ya hadithi

¹⁰³ *Sunan Tirmidhi*, Juz. 5, uk. 26.

¹⁰⁴ *Sahihi Bukhari*, Juz. 4, uk. 264.

¹⁰⁵ *Shi’ah wa Raja’a*, Juz. 2, uk. 161.

Maswali na Majibu

hizo imefanya zigundulike ikhtilafu kadhaa, na baadhi ya ikhtilafu hizo zimetatuliwa, zingine zimetolewa maelezo na makusudio yake, hali kadhalika zingine zinaweka bayana ukamilikaji wa kudhihiri kwa Imam Mahdi [a.s], bila shaka zipo kati ya hizo zinastahili kukosolewa.....”¹⁰⁶

Kwa hakika Allama Twabatwabai amelieleza na kulichambua jambo hilo kwa marefu na mapana, lakini kutokana na kuwa kitabu hiki ni kidogo hatukuweza kutaja na kueleza yote aliyoyaeleza na kuyabainisha.

Swali 24: Je! Ipo ishara yoyote katika vitabu vya Ahlu Sunna kuhusu kuchomwa moto nyumba ya Wahyi [nyumba ya Bi Fatimah] au kugusiwa hilo?

Jibu: Ndio, wapo watu waliojasirika kuangamiza pande la nyama la Bwana Mtume [s.a.w.w], ambaye ni mbora wa wanawake wote wa ulimwengu, naye sio mwingine bali ni Fatimah Zahra [a.s], walitaka kumchoma moto, na jambo hilo halina uficho, kwani upo ushahidi na dalili mbali mbali katika vitabu vya hadithi pamoja na historia, vile vile wapo miongoni mwa wanachuoni wa Ahlu Sunna walioeleza kinaga ubaga suala hilo, na wapo walioandika tukio hilo kama vile lilivyojiri, hali kadhalika wapo walio majasiri na kudiriki kueleza wazi kwamba tukio hilo lilifanywa na Khalifa wa pili kwa sentensi hii: “Alishika kigogo cha moto.”¹⁰⁷

Baadhi yao waliizingira nyumba ya Bibi huyu mtukufu [Fatimah Zahraa] na kuwaweka chini ya ulinzi na wakitishia kuivamia: “Kisha

¹⁰⁶ *Tafsiir Miizan*, Juz. 2, uk. 108.

¹⁰⁷ *Tarikh Twabari*, Juz. 3, uk. 101, *Muswanaf Ibn Abi Shayba*, Juz. 7, uk. 432, *Aqdul-Fariid*, Juz. 4, uk. 260 chapa ya Misri mwaka 1381 na *Ansaabul-Ashraaf*, Juz. 2 uk. 268.

Maswali na Majibu

akasimama Umar bin Khatwab akaenda pamoja na kikosi cha watu mbele ya mlango wa Fatimah..... Umar na wenzake wakabakia hapo hadi walipomtoa Ali”¹⁰⁸

Na wapo waliosukuma mlango na kumgonga Fatimah Zahraa [a.s] tumboni, na hivyo ikawa ndiyo sababu ya kufa kiumbe kilichokuwemo tumboni mwake, na wapo waliothubutu kutaja jina la mtu aliye-fanya hivyo, sio mwingine bali ni Umar bin Khatwab, walisema: Kwa hakika Umar alimpiga Fatimah ubavuni hadi kikafa kiumbe kilichokuwemo tumboni mwake ambaye alikuwa amepewa jina la Muhsin.¹⁰⁹

Wamediriki kumvunjia heshima, kumdhalilisha, kumvunja mbavu, kumjeruhi, kuporomosha ujauzito wake na hata kumnyima urithi wake.¹¹⁰

Na wapo baadhi wanaosema: Umar na Abu Bakr walimuomba radhi baada ya kisanga hicho, wanazuoni hao wa Ahlu Sunna wanaeleza kama ifuatavyo: Umar akasema kumwambia Abu Bakr: Twende kwa Fatimah tukamuombe msamaha hakika sisi tumemuudhi yeye, basi wakaenda pamoja hadi walipofika kwake, hapo wakaomba idhini ya kuingia ndani, basi hakuwapa idhini, hapo wakamwendea Ali wakaongea naye akawaruhusu wakaingia kwa Fatimah, walipokaa akageuza uso wake na kuelekea ukutani, wakamtolea salamu na hakuwarudishia salamu.¹¹¹

¹⁰⁸ *Imama wa Siyasa* Juz. 1, uk. 12.

¹⁰⁹ *Siyar Aalam Nubalaa*, Juz. 15, uk. 578, *Lasanul-Miizan*, Juz. 1, uk. 373 na *Miizanul-I'tidal*, Juz. 1, uk. 139.

¹¹⁰ *Faraaid Simtaini*, Juz. 2, uk. 34, Jawiini Shafii aliyekufa mwaka 722, Shamsu Diin Dhahabi.

¹¹¹ *Imama wa Siyasa*, Juz. 1, uk. 12.

Maswali na Majibu

Dhahabi anasema: Abu Bakr alikwenda nyumbani kwa Fatimah ili kumuomba radhi, Ali akamwambia Fatimah: huyu hapa Abu Bakr anaomba idhini ili aingie kwako unamruhusu? Fatimah akasema: “Ndio, basi akamruhusu kuingia, kisha akaomba amridhie”¹¹² na ¹¹³

Baadhi ya waandishi walieleza bayana majuto ya Khalifa wa kwanza Abu Bakr Swiddiq pindi alipokaribia kufariki, alijutia kitendo chake kibaya alichokifanya cha kuchoma moto nyumba ya Wahyi, alisema: “Laiti ningeliacha kuichoma moto nyumba ya Fatimah ningekuwa nimefunga mlango wa vita, lakini kwa kitendo kile nimetangaza vita.”¹¹⁴

Swali 25: Je! Zipo ibara na maelezo ya vitabu yaliyobadilishwa, kupotoshwa au kugeuzwa kabisa kuhusiana na jambo hilo?

Jibu: Bila shaka zipo baadhi ya ibara na maelezo yaliyobadilishwa na hata mengine kufutwa, kwa mfano ibara zilizopo katika kitabu *Al-Aqdul-Fariid* cha Ibn Abdu Rabih Andalusi, imedhihiri kwamba baadhi ya ibara hazijabadilishwa, kwa mfano ibara hii: Abu Bakr alimtuma Umar awatoe waliokuwemo ndani ya nyumba ya Fatimah, akamwambia: Iwapo watakataa basi waue, hapo akachukua kigogo cha moto ili akachome nyumba yao, njiani akakutana na Fatimah akasema: Ewe Ibn Khatwab umekuja ili kuchoma nyumba yetu?

¹¹² *Siyar Aalaam Nubalaa*, Juz. 2, uk. 121.

¹¹³ Zingatia maneno ya Dhahabi kwamba anaomba radhi kutokana na kunukuu tukio hilo la kuhuzunisha, na katika toleo lingine maelezo hayo hayapo.

¹¹⁴ *Mu'ajamul-Kabiir*, Juz. 1, uk. 62 hadithi nambari 43, *Kitabul-Amuwwaal bin Salaam* uk. 174 aliyefariki mwaka 224 H, ibara hiyo imebadilishwa na mahala pake yapo maneno haya “kadhaa wakadha.”

Maswali na Majibu

Akasema: “Ndio, au mkubali yale Umma uliyokubaliana nayo.”¹¹⁵

2. Ama katika kitabu Mashuhuri cha Ibn Qutayba ibara hii imefutwa: “Hakika Muhsin aliporomoka kutokana na pigo la Qunfuz Al Aduwi.”¹¹⁶

3. Upotoshaji katika kitabu *Muruuj Dhahab* Juz. 3, uk. 86 chapa ya Maymuuniya imekuja kama ifuatavyo: Urwat bin Zubeir katika hali ya kutetea tendo la kaka yake anasema hivi: Abdullah bin Zubeir na Bani Hashim katika bonde walilozuiliwa walitishiwa kuchomewa moto, na wakati huo huo Umar bin Khatwab kuhusiana na Bani Hashim katika kutoa kiapo cha utii kwa Abu Bakr wakaenda kinyume, hivyo ndivyo alivyofanya, yaani alikusanya kuni na kuchoma moto nyumba yake, ama katika chapa mpya ibara hizo akazifuta, lakini pamoja na upotoshaji wote huo bado yapo katika vitabu vya makundi yote ya kiislamu ambayo yamenukuu mambo hayo, kwani wapo wale ambao hawakutaka kubadilisha ukweli na haki.

Kuhusiana na mchakato huu wa uchomaji moto nyumba ya Wahyi nataja baadhi ya vitabu rejea ambavyo kwa njia moja au nyingine vimesimulia tukio hilo navyo ni:

Ithbatul-Wasiya uk. 143, *Al-Waafi bil Wafayaat*, Juz. 6 uk. 17, *Al-Khatwat*, Juz. 2, uk. 346, *Al Farqu Baina-Firaq* uk. 148, *Milal wa Nihal* Juz. 1, uk. 57, *Shaafii* Juz. 4, uk. 120, *Sharh Ibn Hadiid* Juz. 14, uk. 193 na Juz. 2, uk. 60, *Bihar Anwar*, Juz. 28, uk. 270 na Juz. 30, uk. 284, *Talkhisu Shaafii*, Juz. 3, uk. 156, *Taqriib Ma'arif*, uk. 23,

¹¹⁵ *Aqdul-Fariid*, Juz. 4, uk. 260.

¹¹⁶ *Kifayatul-Twaalib* uk. 413, *Manaqib* uk. 407 hadithi ya 3 [yaani ujauzito wa Bibi Fatimah Zahraa uliopewa jina la Muhsin uliporomoka kutokana na pigo la Qunfuz Aduwi].

Maswali na Majibu

Taraaif, uk. 274 na *Ma'asat Zahraa* na vinginevyo.

Tunamshukuru Mola Muweza kwa kutuwezesha kueleza baadhi ya matukio muhimu, dondoo na vidokezo kadhaa ndani ya kitabu hiki kidogo, tunawaasa wapendwa wasomaji kusoma na kuzingatia yale yaliyoelezwa, aidha tupo mbioni kujibu maswali hayo na yanayofanana na hayo kwa urefu, mapana na kwa kina zaidi katika matoleo yajayo akipenda Mwenyezi Mungu, kwani huwatatiza baadhi ya watu, ee Mwenyezi Mungu tujaalie hilo.

**Wassalaamu Alaykum
Najmu Diin Muruji Twabasi.**

Maswali na Majibu

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi

Maswali na Majibu

24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto

Maswali na Majibu

54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume
Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia
iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihii zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

Maswali na Majibu

82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqaalain
102. Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)

Maswali na Majibu

109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi

Maswali na Majibu

134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kibusunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kibusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kibusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini ni swala ya Jamaa

Maswali na Majibu

BACK COVER

Kitabu hiki kidogo kiitwacho *Maswali na Majibu* kimekusanya baadhi ya majibu ya maswali aliyoulizwa mtunzi katika hadhara na vikao kadhaa mbalimbali ambavyo alishiriki kujibu maswali hayo. Kisha kamati maalumu ikakaa na kuandaa na hatimaye kuwa kitabu. Hivyo, kimeandaliwa kwa muhtasari sana pamoja na kutaja vitabu rejea vinavyotegemewa zaidi na Ahli Sunna ili watu wengi wapate faida.

Matumaini yetu ni kwamba baada ya mpendwa msomaji kusoma na kuelewa vizuri utawafikishia wengine, na iwapo utapatikana utata au kutofahamika baadhi ya mambo unaweza kuwasiliana nasi. Matarajio ya hapo baadaye ni kujibu maswali hayo na yanayofanana na hayo kwa mapanana marefu na ufafanuzi zaidi.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Al-Itrah Foundation

S.L.P. - 19701,

Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu / Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.alitrah.org

Katika mtandao: www.alitrah.info

Maswali na Majibu
